

JAMHURI YA MUUNGANO WATANZANIA  
WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI  
(Jeshi la Magereza)

Anwani ya Simu: NIL  
Simunamba: NIL  
Email: NIL



MKUU WA MAGEREZA KILINDI,  
S.L.P 01  
SONGE- KILINDI.  
02/2/2024.

TAARIFA KWA UMMA KUHUSU NAFASI ZA AJIRA ZA JESHI LA MAGEREZA KWA  
MWAKA 2024

1. Kufuatia mkakati wa Serikali wa kuimarisha utendaji wake imetoa fursa ya ajira kwa Wizara ya Mambo ya ndani Jeshi la Magereza. Hivyo Kamishna Jenerali wa Jeshi la Magereza anatangaza nafasi za ajira za kujiunga na Jeshi la Magereza kwa mwaka 2024 kwa Vijana wenye elimu ya kidato cha nne (FORM IV), Jeshi litaajiri kwa kuzingatia vigezo vinavyohitajika kulingana na maelekezo ya Serikali. Hivyo waombaji wote wanaotaka kujiunga na Jeshi la Magereza wanatakiwa wawe na sifa zilizoainishwa hapa chini.

(I) SIFA ZA MWOMBAJI WA ELIMU YA KIDATO CHA NNE (WASIO NA UJUZI)

- ❖ Awe ni raia wa Tanzania
- ❖ Awe na kitambulisho cha uraia au namba za Utaifa kutoka Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA)
- ❖ Awe amehitimu Mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) au waliopo Makambini.
- ❖ Asiwe amewahi kuajiriwa Serikalini
- ❖ Awe na umri kati ya miaka 18 - 25
- ❖ Awe na Cheti cha Kuzaliwa
- ❖ Awe na siha na afya njema ya mwili na akili iliyothibitishwa na Daktari wa Serikali.
- ❖ Asiwe ameo /Kuolewa
- ❖ Asiwe na alama au michoro yoyote katika mwili (tattoo)
- ❖ Awe na urefu usiopungua futi 5'4" kwa wanawake na futi 5'7" kwa wanaume.
- ❖ Awe na nidhamu na tabia njema na awe hajawahi kupatikana na hatia kwa shitaka la Jinai Mahakamani na hajawahi kufungwa.
- ❖ Awe tayari kujigharamia yeye binafsi katika hatua zote za awali za usaili wa ajira hii hadi kuripoti chuoni.
- ❖ Awe tayari kuhudhuria mafunzo ya awali ya Askari Magereza na kufanya kazi mahali popote nchini Tanzania.

(II) UTARATIBU WA KUTUMA MAOMBI NI KAMA IFUATAVYO:-

Waombaji wote waandike barua kwa Mkuu wa Gereza Kilindi. Vile vile barua hiyo ya maombi iandikwe kwa mkono (handwriting) na namba ya simu ya mkononi inayoweza kupatikana muda wote.

Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 06 FEBRUARY 2024.


(III) BARUA ZA MAOMBI ZIAMBATANISHWE NA NAKALA ZIFUATAZO:

- ❖ Nakala ya cheti cha kuzaliwa (Birth Certificate)
- ❖ Nakala za vyeti vya kuhitimu Kidato cha Nne (Academic Certificate na Leaving Certificate)
- ❖ Cheti cha uthibitisho wa Siha njema kutoka kwa Mganga wa Serikali.
- ❖ Nakala ya kitambulisho cha uraia au namba ya utaifa kutoka Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA)
- ❖ Nakala ya Cheti cha kufuzu Mafunzo ya Jeshi la kujenga taifa (JKT) au Barua ya Utambulisho kutoka kwa Mkuu wa Kikosi kwa waliopo Kambini
- ❖ Picha moja (01) ya Passport size
- ❖ Barua ya utambulisho kutoka kwa Afisa Mtendaji wa Kijiji/Mtaa anakoishi mwombaji.

(IV) ZINGATIA

- (a) Waombaji wote ambao walishafukuzwa katika kozi za mafunzo ya awali ya uaskari Magereza hawaruhusiwi kuomba tena.
- (b) Mwombaji yoyote atakayewasilisha nyaraka za uongo/kughushi (Forged Documents) atakuwa ametenda kosa la jinai hivyo atachukkuliwa hatua kali za kisheria.

Imetolewa na



A/INSP M.D.KAZAWADI  
MKUU WA MAGEREZA (W) KILINDI

**MKUU WA GEREZA  
WILAYA (DPO)  
S.L.P.01  
KILINDI**

Nakala : Mkuu wa Wilaya Kilindi  
DSO- Kilindi  
OCD - Kilindi